

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA SITA

09 APRILI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA SITA – TAREHE 09 APRILI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA)

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Mzumbe kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 (*The Annual Report and Audited Accounts of Mzumbe University for the Year ended 30th June, 2017*).

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

43. MHESHIMIWA DKT. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kauli Mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ni pamoja na kuongeza uwekezaji kwa kuvutia Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa vikwazo vinavyoathiri dhana hiyo vinaondolewa.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

44. MHESHIMIWA JUSTIN JOSEPH MONKO (SINGIDA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Tarafa ya Mtiko katika Jimbo la Singida Kaskazini yenye Kata 6 haina Kituo cha Afya cha Serikali:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kukamilisha Jengo la Kituo cha Afya katika Kata ya Makuro

lililojengwa na Wananchi ili Wananchi waweze kupata huduma za rufaa kutoka katika Zahanati zilizopo;

(b) Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha za majengo ya ziada katika Kituo cha Afya Kata ya Makuro ili kutoa huduma bora kwa Wananchi.

**45. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kwa muda mrefu sasa Mkuu wa Wilaya ya Ikungi amekuwa akijichukulia Sheria mkononi na kuwanyanyasa Wananchi wa Kata za Ighombwe, Iglansoni na maeneo mengine ya Wilaya ya Ikungi:-

Je, Serikali inaweza kutoa majibu ni mamlaka yapi aliyonayo Mkuu wa Wilaya huyo ya kuwanyanyasa na kuamrisha mali za Wananchi kuchomwa moto au kuporwa na Serikali bila utaratibu wowote wa kisheria kwa kisingizio kuwa wanaishi maeneo yasiyoidhinishwa kwa makazi.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**46. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na ongezeko la Wasichana wanaokatishwa Shule kwa sababu ya mimba.

47. MHESHIMIWA BERNADETHA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Miundombinu ya Shule ya Sekondari Rugambwa ilijengwa mwaka 1964 na Sekondari ya Bukoba imejengwa mwaka 1939 hivyo imechakaa sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati Shule hizo.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

48. MHESHIMIWA ANTHONY CALIST KOMU (MOSHI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya mara kwa mara ya kuyapima upya mashamba

yaliyotaifishwa wakati wa Azimio la Arusha ambayo hivi sasa yamebadilishwa matumizi na kujengwa Shule, Zahanati, Hospitali, makazi n.k.

**49. MHESHIMIWA SONIA JUMAA MAGOGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wananchi wa Wilaya ya Handeni ambao wanakosa ardhi ya kuendesha shughuli zao za kilimo kwa sababu ya kumilikiwa na wachache.

WIZARA YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

**50. MHESHIMIWA ESTER ALEXANDER MAHAWE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:- Mkoa wa Manyara hususani Wilaya ya Mbulu imewahi kutoa Wanariadha mahiri ambao walililetea Taifa heshima kubwa, lakini cha kushangaza Wanariadha hao wametelekezwa.

(a) Je, ni lini Serikali sasa itaandaa utaratibu wa kuwaenzi Wanariadha hao;

- (b) Je, ni lini sasa Serikali itajenga uwanja kwa ajili ya riadha katika Mkoa wa Manyara ili kuwahamasisha Wanariadha wapya.

WIZARA YA MADINI:

51. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-
Wananchi wa Msalala wengi wao ni Wachimbaji wadogo lakini hawana maeneo ya kufanyia kazi, maeneo mengi ya kufanyia kazi yana leseni za Wachimbaji wakubwa na hawazifanyii kazi:-

- (a) Je, kuna leseni ngapi za utafiti wa madini zilizotolewa kwa maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala;
- (b) Je, ni maeneo gani Serikali inadhamiria kuyatoa kwa Wachimbaji wadogo wa Msalala;
- (c) Je, kwa kuanzia, Serikali inaweza kuwaruhusu Wananchi wafanye uchimbaji mdogo kwenye maeneo ya reef 2, Kijiji cha Kakola namba Tisa, Kata ya Bulyanhulu, Bushimangila na Msabi Kata ya Mega na Lwabakanga na Nyangalata Kata za Lunguya na Bulyanhulu.

52. MHESHIMIWA OSCAR RWEGASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-
Wananchi wa Kijiji cha Busiri Wilayani Biharamulo
ni miongoni mwa Watanzania ambao
wanaendesha maisha kwa shughuli za uchimbaji
mdogo kama ilivyo kwa wenzao wengi na
kwingineko nchini. Uchimbaji mdogo wa Busiri
unahitaji kuungwa mkono na Serikali kimkakati:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaunga
mkono Wachimbaji wadogo wa Busiri na ni upi;
- (b) Je, Serikali ipo tayari kuwatembelea Wananchi
wa Kijiji cha Busiri ili kuwaelewesha ni namna
gani itanza utekelezaji wa mpango huo wa
kuwaunga mkono Wachimbaji hao.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya
Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa
Mwaka wa Fedha 2019/2020.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
09 APRILI, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**